



<https://habarileo.co.tz/habari/2020-10-135f859f025512e.aspx>

Duwasa kutumia bilioni 2.4/- kuchimba visima

Tanzania Standard Newspapers Ltd (Magnus Mahenge, 14/10/2020)

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Dodoma (Duwasa) itatumia Sh bilioni 2.4 kuchimba visima virefu vya maji katika maeneo mbalimbali kuzunguka jiji hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa Duwasa, David Pallangyo, alisema wakati akizungumza katika eneo la kuchimba Mtaa wa Chilwana, Kata ya Ihumwa jijini hapo kuwa, mamlaka hiyo imepokea Sh bilioni moja kutoka serikalini kupitia Wizara ya Maji na uchimbaji umeanza.

Alisema imeanza kuchimba visima vitano hadi sita vitakavyoongeza ujazo wa maji kwa mita 3,000 kwa siku kama mkakati wa muda mfupi kwa ajili ya kutatua changamoto ya maji wakati mipango ya muda wa kati na mrefu ikiendelea.

Tayari uchimbaji wa kisima cha kwanza umefikia mita 82 kati ya 150 katika Mtaa wa Chilwana, Kata Ihumwa ili kupunguza adha ya ukosefu wa maji katika maeneo ya Mwangaza, Ihumwa na Njedengwa.

Maji kutoka katika visima hivyo yatasafirishwa umbali wa kilometa 12 hadi lilipo tangi la Njedengwa na hadi kufikia Desemba, mwaka huu watakuwa wamekamilisha uchimbaji na maji kufika eneo hilo ili kusaidia mahitaji ya watu na biashara.

Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Antony Sanga, alisema serikali imeshatoa Sh bilioni moja kati ya bilioni 2.4 zilizoombwa na Duwasa kuondoa changamoto ya maji maeneo ya pembezoni mwa jiji.

Sanga alisema, serikali imetoa fedha hizo kwa kuwa inataka kupunguza changamoto ya maji katika kipindi kifupi wakati mikakati ya muda wa kati na mrefu ikiandaliwa.

Mkakati wa muda wa kati ni kuleta maji kutoka katika Bwawa la Farkwa na mkakati wa muda mrefu ni kuleta maji kutoka katika Ziwa Victoria. Tayari usanifu wa awali umefanyika utafuata usanifu wa kina.

Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Josephat Maganga, alisema Mji wa Dodoma unakua kwa kasi kiutawala na kibiashara, hivyo huduma za maji zinahitajika kwa ajili ya maendeleo ya watu hao.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk Binilith Mahenge baada ya kukagua mtambo wa Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DCCA), alisema uwepo wa huduma muhimu za kijamii unachangia wawekezaji kufika na kuwekeza katika jiji hilo.

“Miongoni mwa huduma hizo muhimu ni pamoja na uwepo huduma za maji, miundombinu ya barabara, uwepo wa elimu bora, huduma za afya na umeme,” alisema.

Kuhusu utoaji wa fedha kwenye sekta ya maji alisema, Rais John Magufuli alitoa fedha kwa ajili ya kununua mashine mpya mbili baada ya zile za awali kuzimika kwenye vyanzo vya Mzakwe na sasa maji yanapatikana kwa urahisi katika mji wa serikali.

Dk Mahenge alisema Rais Magufuli ameendelea na mkakati wa kutoa fedha ili kuhakikisha huduma za maji zinapatikana kwa kuchimba visima katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya Michese, Mkonze, Njuguni na Ndachi.

Aliagiza Duwasa kuhakikisha uchimbaji visima hivyo unakamilika ndani ya miezi miwili.